**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (OR-TAMISEMI)**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA**
**SHULE YA SEKONDARI NJINJO**

Blogu: njinjosec.blogspot.com Barua pepe: njinjoss@gmail.com

Ofisi ya Mkuu wa Shule
S.L.P 119, **KILWA MASOKO.**
SIMU: 0685 306666

DC/NJSS/F2/2020/01

JINA LA MWANAFUNZI ..............................................................................................
KWA MZAZI /MLEZI WAKE

Ndugu,

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI NJINJO MWAKA 2021**

Ninayo furaha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza (1) katika shule hii na masomo yataanza tarehe 11/01/2021, **mwisho wa kuripoti shuleni ni siku 14 tangu kufungua, baada ya hapo mwanafunzi hatapokelewa na hatua za kisheria zitachukuliwa kwa mzazi kwa kukwamisha maendeleo ya elimu nchini. Kutakuwa na kozi maalumu ya kiingereza na itaendeshwa kwa kipindi cha wiki sita za mwanzo hivyo wanafunzi wote wanatakiwa wawahi kuripoti shuleni kwani kozi itaanza tarehe 11-01-2021.**

Shule ipo mkoa wa Lindi, Wilaya ya Kilwa, Tarafa ya Njinjo, kata ya Njinjo, kijiji cha Kipindimbi mita 1750 kutoka barabara ya Nangurukuru-Liwale

Kauli mbiu yetu ni **"Education for Bright future" maana yake Elimu kwa baadaye angavu.** Unapokuja shule hii utafakari namna utakavyoifaidi kauli hii na kunufaisha Taifa kwani utakuwa umeanza kuyang'arisha maisha yako ya baadaye.

*Nakukaribisha sana shule ya sekondari Njinjo kutumia fursa hii adhimu kwa ajili yako, familia na Taifa*

**KAPAGI, P.K**
**MKUU WA SHULE**

**A: MAHITAJI YA LAZIMA**

**1. SARE ZA SHULE**

i. **Kwa wavulana**:

**a.** Aje na suruali mbili za bluu bahari ndefu, zenye marinda na tanap pana(inch 20) zisizo nyembamba (Suruali nyembamba maarufu kama modo zitachanwa kwani haziruhusiwi kabisa).

**b.** Aje na mashati mawili meupe ya tomato mikono mifupi yenye ukosi (*kola*) shingoni.

**c.** Soksi rangi nyeusi jozi mbili na Tai ndefu ya rangi ya bluu bahari

**d.** Aje na viatu vya ngozi vyeusi jozi mbili vya kawaida visivyo na soli ndefu wala kuchongongoka mbele. (viatu vya plastic havitapokelewa)

ii. **Kwa Wasichana**:

**a**. Aje na sketi mbili za bluu bahari ndefu za kupita magoti na za rinda boksi zisizo na mikanda.

**b**. Aje na mashati mawili meupe ya tomato mikono mifupi yenye ukosi (*kola*) shingoni, waislamu wanaweza kushona nusu kanzu kwa kitambaa cha koshibo na hijabu safi ya kushona kwa kitambaa cha halua. **(Izingatiwe kwamba hijabu si sare ya lazima lakini anayehitaii kutumia lazima avae ya kushona maridadi, nyeupe ndefu na isiyoacha mabega wazi, ni kosa kushindwa kuripoti shule kwa sababu ya hijabu)**

**c.** Soksi rangi nyeupe jozi mbili na Skafu ya rangi ya bluu kwa wasiovaa hijabu

**e.** Aje na viatu vya ngozi vyeusi jozi mbili vya kawaida visivyo na soli ndefu wala kuchongongoka mbele ( viatu vya plastic hasa bajaji havitapokelewa)

*MUHIMU: Suruali na sketi zishonwe kwa kufuata kitambaa cha mfano kilichoambatanishwa na si vinginevyo, kinyume na hapo hazipokelewa. Mashati yashonewe alama ya I bega la kushoto ili kutambulisha kidato.*

**2. SARE MAALUM NA ZA MICHEZO**

iii. Awe na fulana ya rangi ya bluu yenye yenye kola na nembo ya shule(huvaliwa jumatano) ambazo hupatikana shuleni, pia sweta la rangi ya bluu sawa na fulana lakini yenye kola ya V( kwa wanaopenda masweta)

iv. Nguo za michezo bukta (wavulana) Track (wasichana) na fulana za bluu(Jezi) na na raba nyeusi jozi moja.

v. Wanafunzi wa Hosteli washone magauni 2 mtindo wa solo kwa kitambaa kizito cha Bluu nyeusi(Dark Blue)

**3. MAHITAJI KWA AJILI YA TAALUMA**

vi. Madaftari 13 kati yake 12 yafaa yawe ya kaunta kuanzia 2quare, begi na kalamu za wino za kutosha pamoja, mkebe wenye vifaa vya kufanyia hesabu (*mathematical set*) na kamusi ya kiingereza-Kiswahili.

vii. Mafaili 2 moja kwa ajili ya taarifa za mwanafunzi na lingine kwa ajili ya Benki ya maswali.

viii. Karatasi nyeupe Rimu 1 kwa ajili ya majaribio na mitihani ya nusu muhula ili itolewe kwa kiwango(standard)

**4. MAHITAJI YA USAFI, ELIMU YA KUJITEGEMEA NA MAZINGIRA**

ix. Mvulana aje na fagio la chelewa, Ndoo ndogo, Panga na kwanja(fyekeo) vilivyonolewa na Msichana Aje na Fagio la chelewa, ndoo ndogo, Jembe, na mfagio laini/brush(Soft bloom).

x. Shule ina hosteli ya wasichana na chakula cha mchana kwa wanafunzi wa kutwa, maelekezo yanapatikana shuleni.

**B: HATI ZA LAZIMA**

**i.** Nakala(Copy) ya cheti cha kuzaliwa au FOMU YA KIAPO CHA URAIA kwa wasio na cheti cha kuzaliwa.

**ii.** Cheti cha Hospitali *(Request for Medical examination*) mwanafunzi apimwe na mganga kwenye hospitali ya serikali.

**iii.** Fomu ya maelezo binafsi ya mwanafunzi na mzazi.

**C: MAMBO YA KUZINGATIA**

i. Mwanafunzi hatakiwi kubadili jina,Jina litakalotumika ni lile alilofanyia mtihani wa darasa la saba.

ii. Iwapo mzazi au mlezi atabadili anuani na namba ya simu ni muhimu aijulishe shule ili iwe rahisi kufanya mawasiliano.

**D. KANUNI ZA SHULE**

**i. HESHIMA**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuzingatia yafuatayo:

1. **Kusimama na kumsalimu mwalimu au mtu yeyote aliyewazidi umri anapopita, anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.**
2. Kutotumia lugha mbaya, wakati wowote kati yao wenyewe, kwa walimu na kwa watu wengine.
3. Kuwaheshimu wafanyakazi wote walioko shuleni kama walezi wake.
4. Kushirikiana na kusaidiana na wanafunzi wenzake katika kazi.
5. Kuthamini na kuheshimu kazi za aina zote.
6. Kuwa na kucha fupi zisizopakwa rangi na nywele fupi pia ziwekwe katika hali ya usafi kila wakati, kuvaa mavazi ya heshima.
7. Kuitika mara moja na kukimbilia aliko Mkuu/mwalimu anayekuita.
8. Kuheshimu bendera ya serikali, picha za viongozi wa serikali, nembo ya Taifa "coat of Arms", wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.
9. Kuheshimu ukumbi wa mikutano, mahali pa kulia chakula, ofisi za shule, mali ya binafsi na mali ya umma.
10. Kusimama katika mstari wakati wa kupokea huduma.
11. Kuwa mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote ulipo.
12. Kunyosha mkono juu na asimame anapouliza na kujibu maswali.
13. Kukaa kimya wakati wote anapokuwa darasani, asitoke bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyeko.
14. **Ni marufuku kwa mwanafunzi kuleta** vifaa vifuatavyo shuleni **SIMU au KIFAA CHOCHOTE CHA SIMU, Pasi ya umeme, Camera, "Heater", VYAKULA** vya aina yoyote.

**ii. MAHUDHURIO**

Kila mwanafunzi anatakiwa:

1. Kuhudhuria shule muda wote wa masomo, vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa.
2. Kuhudhuria katika kazi zote za mikono, mikutano ya shule kama baraza la shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha bendera ya Taifa, mikutano ya Bweni na madarasa.

**iii. HOSTELI NA MAANDALIO YA JIONI**

**1.** Shule inayo hosteli kwa wanafunzi wa kike watakaowahi na watakaokidhi vigezo ikiwemo kuchangia chakula cha miezi 3

**2.** Kila mwanafunzi anayekaa hosteli au jirani na shule anatakiwa ahudhurie maandalio ya jioni kuanzia Jumatatu hadi Jumamosi saa 1.30 hadi saa 4.00 usiku. **Mwanafunzi harushusiwi kukaa au kulala hosteli au nyumbani muda huu ukipatikana adhabu itatolewa zidi yako.**

**iv. MAENDELEO YA MWANAFUZI KITAALUMA NA TABIA**

Shule hutuma taarifa za maendeleo ya mwanafunzi kitabia na kitaaluma kila muhula, tafadhali mzazi/mlezi hakikisha unaipata na kumshauri mwanao kuhusu maendeleo yake.

**v. KUWAHI**

Kila mwanafunzi anatakiwa:

1. Kuthamini muda na kuwahi katika shughuli zote za shule kama zilivyopangwa.
2. Kufika shuleni kwa tarehe zilizopangwa kufuatana na muhula husika. Mzazi pia atawajibika kwa utoro.

**E. SARE YA SHULE**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa katika sare ya shule wakati wote wa:

1. Masomo darasani, Baraza la shule na Michezo.
2. Kutoka nje ya shule Kwa shughuli za kishule.

3. Kwenda hospitalini ikiwa atatokea shule.
4. Wanaposafiri kuja shuleni au kwenda makwao wakati wa likizo (hasa wa hosteli).
5. Mtindo wa kunyoa ni sehemu ya sare ya shule na kila mwanafunzi atanyoa saizi moja isiyozidi kitana kidogo, asitie dawa yoyote ikiwemo wevu na blaki. Panki na mitindo mingine hairihusiwi kabisa

**NB:** Mwanafunzi haruhusiwi **kujaa na nguo za nyumbani** nje ya zile ulizoagizwa na shule au **kuvaa kofia, mizura, nguo fupi, zenye mipasuo, milegezo, modo, kufuga kucha ndefu, kupaka rangi kucha na midomo, kuvaa heleni, mikufu, bangili, nguo za kubana, viatu vyenye visigino virefu, mapambo mengine yoyote pamoja na sare akiwa shuleni.**

**F. MIPAKA YA SHULE**

Kila mwanafunzi azingatie mipaka ya shule kama ifuatavyo:

1. Ni kosa kwa mwanafunzi kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali cha Mkuu wa shule.
2. Haruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali/ruhusa maalum:

i. Chumba cha walimu (staffroom). ii. Ofisi za shule. Iii. Maabara. iv. Jikoni. V. Nyumba za walimu

**G. UGONJWA**

1. Tafadhali mzazi/mlezi unatakiwa kufanya **uchunguzi wa kina wa Afya ya mwanao kabla hajaripoti** shuleni na wakati wa likizo ili kuepuka usumbufu wakati wa masomo.
2. Endapo kutakuwa na tatizo lolote la kiafya mwanafunzi atatakiwa kutoa taarifa kwa mwalimu wa zamu, mwalimu wa darasa, kwa matroni wa shule, mwalimu mlezi n.k.
3. Mwanafunzi mgonjwa hataruhusiwa kupumzika shuleni atatakiwa kupelekwa kituo cha afya, aidha ikiwa ataugua akiwa nyumbani ni lazima aende kwanza kituo cha afya kabla ya kufika shuleni.
4. Mwanafunzi mwenye matatizo lazima aufahamishe uongozi wa shule au mwalimu wa Afya, mara afikapo shuleni na daktari athibitishe kwenye fomu.

**ANGALIZO KWA MWANAFUNZI**

1. Mwanafunzi harusiwi kuandika maandishi katika dawati, meza, viti, vitabu au kwenye kuta za majengo ya shule. **Akifanya hivyo atalazimika kugharamia box la chaki, rangi, saruji na fundi kukarabati.**
2. Ni kosa kwa mwanafunzi kukutwa na kitu chochote kinachohusisha mapenzi mfano barua, daftari lenye nyimbo za mapenzi n.k.
3. Ni kosa kwa mwafunzi kupita eneo lisilo na barabara maalumu au kutupa takataka maeneo yasiyo rasmi au kuziona takataka bila kuziondoa, hii ni kwa ajili ya kutunza mazingira ya shule.

**j. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE BILA ONYO**

(i) Wizi
(ii) Uasherati, ubakaji, ushoga, ulawiti na usagaji.
(iii) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya, biashara ya madawa yote ya kulevya.
(iv) Makosa mengine ya Jinai.
(v) Kupigana au kupiga mwanafunzi mwenzake, au mtumishi
(vi) Kuharibu mali ya umma na ya watu wengine.
(vii) Kudharau Bendera ya Taifa, Picha za viongozi wa Taifa, Nembo, Wimbo, fedha za Taifa
(viii) Kuoa au kuolewa.
(ix) Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
(x) Kutoa au kushawishi kutoa mimba.
(xi) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni.
(xii) Kukataa adhabu halali.
(xiii) Kujiachisha shule mwenyewe

**FOMU YA KIAPO CHA URAIA.**

JINA LA MWANAFUNZI ..............................................................................................
SHULE ATOKAYO ............................................................................................................
NAMBA YA MTIHANI ......................................................................................................
MIMI MZAZI/MLEZI WA MTOTO ...................................................................................
NAAPA KWA MOYO WA DHATI NIKISEMA KWAMBA MIMI
.......................................................................................... KAZI YANGU
........................................................ NINAISHI KIJIJI
..................................................................................... WILAYA.................................. MKOA
.........................................TANZANIA

KWAMBA MTOTO HUYU ALIYETAJWA HAPO JUU

ALIZALIWA TAREHE ..........................................
KATIKA KIJIJI/MTAA WA ..............................................
WILAYA YA ..................................................................MKOA ...........................................

NA KWAMBA NILIKUWA NIKIISHI KIJIJI HIKI/MJI HUU WAKATI WA KUZALIWA

KWAKE NA NAIKUMBUKA VEMA SIKU HIYO.

KWAMBA TAREHE NA MAHALI ALIPOZALIWA HADI KUANDIKISHWA KWA MUJIBU WA SHERIA KATIKA MUDA WA MIEZI MITATU KWA KUWA HAIKUWEPO SHERIA ZA LAZIMA KWA JAMBO HILI.

AMEAPISHWA MBELE YANGU SAA................. TAREHE ...................................... SIKU .................................. MWEZI .............................................. MWAKA............................

.......................................
**MKUU WA WILAYA**
**(OFFICIAL STAMP)**

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (OR-TAMISEMI)**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA**
**SHULE YA SEKONDARI NJINJO**
Blogu: njinjosec.blogspot.com Barua pepe: njinjoss@gmail.cor

Ofisi ya Mkuu wa Shule
S.L.P 119, **KILWA MASOKO.**

SIMU: 0685 306666

**TAARIFA MAALUMU KUHUSU MWANAFUNZI**

**SEHEMU A.**

Jina kamili (Herufi kubwa)..........................................................................................................
Tarehe ya kuzaliwa .............................................. Kabila ........................... Dini .............................................
Jina la baba ........................................................................................................Anaishi (........) Amefariki (……)
Anuani ya nyumbani/Kijiji ................................................ Kata ......................................... Tarafa
............................................ Wilaya ...................................... Mkoa ............................................

SEHEMU B.

Kazi ya Baba ................................................... Namba ya simu ...............................................................
Jina la mama .......................................................... Anaishi/Amefariki ...........................................................
Kazi ............................................................... Namba ya simu .................................................................

**SEHEMU C. NDUGU KUFUATA UMRI WAKO (KAKA NA DADA )**

| NA | MAJINA YA NDUGU | KIWANGO CHA ELIMU | ANWANI YAKE |
|---|---|---|---|
| 1 | | | |
| 2 | | | |
| 3 | | | |
| 4 | | | |

**SEHEMU D. MICHEZO NA NGOMA UNAZOZIPENDA**

| JINA LA MCHEZO AU NGOMA | SHULE AU MAHALI | TOKA | MPAKA |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |

SEHEMU E.

| MADARAKA AU KAZI | SHULE AU MAHALI | TOKA | MPAKA |
|---|---|---|---|
| | | | |

SEHEMU F.

Mambo unayopenda nje ya masomo *(michezo,mpira,Bustani,kushona)*

*1.* ............................................................ 2. .......................................................... 3. .............................................................

Ninaahidi kuwa na tabia nzuri, mchapakazi na mwenye bidii ya masomo.

Sahihi ya mwanafunzi ..........................................................................................
Tarehe…………………………………………….

Ofisi ya Mkuu wa Shule
S.L.P 119, **KILWA MASOKO.**

SIMU: 0685 306666

## UTHIBITISHO WA MZAZI /MLEZI.

i. Mimi........................................................................Mzazi/Mlezi wa............................................................... ninakubali mtoto wangu asome katika shule ya Sekondari Njinjo. Na nitahakikisha kwamba wakati wote mwanangu atakapo kuwa anasoma hapa shuleni;

ii. Atakuwa hana ruhusa ya kwenda katika majumba ya wageni, maeneo ya ulevi, pooltable n.k.

iii. Ninaahidi kumpatia vifaa vyote vinavyohitajika muda wote mpaka amalize masomo yake na kwamba sitoomba uhamisho.

iv. Ninaelewa kuwa nafasi hii ya mtoto wangu kuingia elimu ya sekondari sio haki yake ila ni bahati aliyotunukiwa na Taifa. Kwa jinsi hiyo, ninaahidi kuwa nitahakikisha anafuata sheria zote za shule na pale atakaposhindwa hatua ipasavyo ichukuliwe dhidi yake.

v. Ninaelewa kwamba sawa na waraka wa elimu bila malipo ninao wajibu wa kumsimamia mwanafunzi hivyo basi nitawajibika ikiwa nitashindwa kumsimamia mwanafunzi kwenye makosa ya utoro wa shule ikiwemo kuacha shule. Nitahakikisha kwamba mwanafunzi anahudhuria siku zote za masomo na kwamba akitoroka siku 5 katika mwezi nichukuliwe hatua za kisheria kwa kukwamisha maendeleo ya elimu katika mkoa wangu.

vi. Ninaahidi kumleta shule kwa wakati uliopangwa bila ya kumchelewesha ili asichelewe masomo kila muhula wa shule unapoanza

vii. Mwanangu akiwa shuleni, alelewe katika dini ya ...........................................................................

viii. Anuani yangu ni ........................................... simu ........................................................................

Sahihi yangu mimi kama Mzazi/Mlezi.............................................

Sahihi ya mtoto.............................................

**Tarehe ...........................................**

**THE PRESIDENT'S OFFICE- REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**KILWA DISTRICT COUNCIL**
**NJINJO SECONDARY SCHOOL**

THE HEADMASTER OFFICE,
P.O. BOX 119, **KILWA MASOKO.**
MOBILE : 0685 306666
05/12/2020

**SPECIAL REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATIOI**

The Medical Officer …………………………………

Name of Student …………………………………........... Date ………………… Term ….…… Year …………….. I shall be very grateful if you will kindly examine the above-named student and give us a report regarding his fitness to undertake studies well in our school.

**A: LABORATORY EXAMINATIONS/INVESTIGATION:**

1. x/ray(......) 2. Urine(......) 3. Stool (......) 4. V/D (......) 5. Tuberculosis (T.B) (.......) 6. Physical fitness(......) 7. Pregnancy (.......)

**B: PRELIMINARY INRORMATION BY PUBIL BEFORE THE DOCTOR**

| No | *DISEASE* | *YES* | *NO* | No | *DISEASE* | *YES* | *NO* |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Tuberculosis(T.B) | | | 11. | Epilepsy | | |
| 2. | Pneumonia | | | 12. | Ear,nose and Throat Troubles | | |
| 3. | Asthma | | | 13. | Skin disorders/Diseases | | |
| 4. | Heart trouble | | | 14. | Anemia | | |
| 5. | Recurrent Indigestion | | | 15. | Operations | | |
| 6. | Jaundice | | | 16. | Serious Accident | | |
| 7. | Dysentery | | | 17. | Malaria | | |
| 8. | Kidney and Urinary Trouble | | | 18. | Stomach Troubles | | |
| 9. | Nervous Breakdown | | | 19. | Eye Disorders | | |
| 10. | Diabetes | | | | | | |

**C: VITAL STATISTICS**

Age ……………….. Height ……………… Weight ……………. Blood pressure ………………………. **Vision e.t.c ……………**

**MEDICAL CERTIFICATE:**

We request the medical officer to complete the following:

I have examined the above named student and considered that he is physically fit/unfit for most activities taken at the school as my findings indicated above.

Date: ………………………Station …………………..……………..Dr's Name: ……………………………….Signature …………………

Thank you in advance.

**Kapagi P.K**
**Headmaster,**